

# HALMASHAURI YA WILAYA BARIADI

SHULE YA SEKONDARI DUTWA,

S.L.P 288,

BARIADI.

**14/12/2020**

Ndugu Mzazi /Mlezi .....

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA KWANZA MWAKA 2021**

Nafurahi kukujulisha kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule hii mwaka 2021.

## 1. UTANGULIZI

Ni matumaini yetu kuwa kama mzazi/mlezi utasoma na kuzingatia maelekezo yote ikiwa ni pamoja na kumsaidia mwanao kuzingatia na kutekeleza maelekezo hayo kikamilifu. Pia tunaamini kuwa utashirikiana na uongozi wa shule kumlea mwanafunzi katika maadili mema na kumsaidia kitaaluma muda wote atakapokuwa mwanafunzi katika shule hii.

## 2. KUFUNGUA SHULE

Shule itafunguliwa siku ya jumatatu tarehe 11/01/2021 asubuhi. Siku hiyo mzazi/mlezi ufike na mwanao shuleni bila kukosa ukiwa na mahitaji yote muhimu kama yalivyoainishwa katika maelekezo hayo.

## 3. SARE YA SHULE

### 3.1. WASICHANA

- Blauzi mbili nyeupe za tetroni zenye mikono mifupi na zisiwe za kubana mwili.
- Viatu vya ngozi vyeusi vya kufunika miguu vyenye visigino vifupi na visivyo na urembo wowote.
- Soksi nyeupe ndefu jozi mbili.
- Bukta rangi ya bluu kwa ajili ya michezo.
- Sketi mbili, moja rangi nyeusi na nyingine rangi ya damu ya mzee zenye malinda madogo, ndefu zinazovuka magoti.
- Viatu vya raba rangi yoyote kwa ajili ya michezo.
- T-shirt rangi ya njano.

### 3.2. WAVULANA

- Shati mbili nyeupe za tetroni zenye mikono mifupi na zisiwe za kubana mwili.
- Suruali mbili, moja rangi nyeusi na nyingine rangi ya damu ya mzee zenye malinda mawili na zisizobana mwili. kamwe asije na model (modo).
- Soksi nyeusi ndefu jozi mbili.
- Bukta rangi ya bluu kwa ajili ya michezo.
- Viatu vya ngozi vyeusi vya kufunika miguu vyenye visigino vifupi na visivyo na urembo wowote
- Viatu vya raba rangi yoyote kwa ajili ya michezo.
- T-shirt rangi ya njano.

#### 4. VIFAA / MAHITAJI YA LAZIMA

- Madaftari makubwa 10 au zaidi
- Kamusi ya Kiswahili na kiingereza (Oxford learner's dictionary)
- Mkebe wa zana za Hisabati (mathematical set)
- Kalamu za wino wa blue au nyeusi za kutosha
- Kalamu za risasi

#### 5. WAJIBU WA MWANAFUNZI

- ✓ Kuwahi shuleni na kila anapotakiwa kufanya hivyo
- ✓ Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote
- ✓ Kuvaa sare ya shule wakati wote awapo shuleni inavyotakiwa
- ✓ Kuhudhuria masomo siku zote za masomo
- ✓ Kuwa na nidhamu ya hali ya juu shuleni na mahali pote
- ✓ Kushiriki kikamilifu katika kazi za shule ,michezo na utamaduni
- ✓ Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kuwepo shuleni kama inavyoonesha ratiba ya shule
- ✓ Mwanafunzi sharti aonekane nadhifu wakati wote
- ✓ Mwanafunzi atunze nywele zake zikiwa fupi.Ni marufuku mwanafunzi kuweka dawa (carl au relaxer) kwenye nywele
- ✓ Mwanafunzi haruhusiwi kunyoa kipara ,panki na kutinda nyusi za macho / usoni
- ✓ Mwanafunzi haruhusiwi kupaka rangi mdomoni au kutunza kucha ndefu

#### 6. SHERIA ZA SHULE

Shule hutoa malezi na kusimamia maadili kwa mwanafunzi kwa kupitia walimu na walezi wengine ,ni wajibu wa kila mwanafunzi awapo shuleni ndani au nje ya shule kuonyesha utii,heshima na nidhamu kwa walimu na wafanyakazi wasio walimu.

Wakati wa kuripoti shuleni mwanafunzi atasomewa sheria zote za shule na atatakiwa kuzitii.Makosa ambayo yaweza kusababisha mwanafunzi kufukuzwa shule ni yafuatayo.

- ✓ Wizi ,uasherati ,ubakaji,ushoga na ulawiti.
- ✓ Ulevi wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya.
- ✓ Makosa ya jinai au kuharibu kwa makusudi mali ya umma.
- ✓ Kupigana au kumpiga mwanafunzi ,mwalimu au mlezi wake.
- ✓ Kuo au kuolewa ,kupata mimba au kusababisha mimba na kutoa mimba.
- ✓ Kugoma ,kuchochea migomo au kukataa adhabu iliyotolewa na mwalimu.
- ✓ Utoro wa muda mrefu (utoro sugu).
- ✓ Kuja shuleni na vitu vilivyokatanzwa kama simu za mkononi au vitu vingine visivyofaa.
- ✓ Kukataa kufanya mitihani au mazoezi ya masomo.
- ✓ Kudharau bendera ya Taifa au nyaraka za taifa.

---

MARY A. MAKALWE  
MKUU WA SHULE